# JARIDA LA ACT

**TOLEO NA.** 40|Mei— Agosti 2021

**We Unite . Dialogue . Advocate**

ACT
Agricultural Council of Tanzania

## Masuala ya Utetezi

1. **Utitiri wa vyombo vya uthibiti katika Sekta ya Kilimo Tanzania.**
2. **Udhibiti wenye kuleta tija katika Sekta ya Pamba Tanzania.**
3. **Madhara yatokanayo na Matumizi ya Pembejeo feki/ bandia kwa tija na kipato cha mkulima.**
4. **Umuhimu wa kutumia mbinu ya "mpango wa uwekezaji kwenye zao moja"**

## Yaliyomo

ACT yashiriki Warsha ya Usalama wa Chakula

Siku ya Mkulima Shambani

Kongamano la Chakula la Duniani

Wadau wa Alizeti wa Kutana

Sherehe ya Mavuno Yaadhimishwa

ACT ya Tembelewa na Ubalozi wa Norway

Jukwaa la Wachambuzi wa Sera Lakutana na Kamati ya Bunge

**HII NDO PFS**

## ACT ILISHIRIKI WARSHA KUHUSU USALAMA WA CHAKULA NA VIWANGO

Baraza la Kilimo Tanzania - ACT ilishiriki katika warsha iliyojikita kwenye mada kuhusu "***Usalama wa Chakula na Viwango***" katika zao la mahindi. Warsha hiyo iliandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini (TPSF) na ilifanyika tarehe 21 Mei, 2021 Jijini Mbeya. Ilihudhuriwa na wadau mbali mbali kama vile: wakulima, wanunuzi, wasindikaji, wataalamu, na wafanyabiashara. Warsha hiyo ililenga kuongeza uelewa wa wadau kuhusu madhara ya sumukuvu kiuchumi na kiafya. Katika warsha hiyo, ACT iliwakilishwa na Bibi Laetitia William (Afisa Sera), ambaye aliwasilisha mada kuhusu "***Changamoto ya Sumukuvu kwenye Mahindi, na Madhara yake Kiuchumi***" Aidha, mada ilijikita kwenye mbinu za kupunguza hasara zinazosababishwa na sumu hiyo, na hatua za kuchukuwa. Warsha hiyo ilidhihirisha uhusiano mzuri kati ya ACT na TPSF katika kuelimisha wakulima na wafanyabiashara wa mahindi kuhusu mbinu za kudhibiti sumukuvu inayopunguza ubora wake, na kuathiri biashara ya zao hili ndani na nje ya nchi

## ACT YASHIRIKI SIKU YA MKULIMA SHAMBANI

Tarehe 2 Julai 2021, ujumbe kutoka Sekretariati ya ACT ukiongozwa na Mkurugenzi wa Miradi, Bw. Mark Magila, ulishiriki "***Siku ya Mkulima Shambani***" Jijini Arusha. Tukio hilo ambalo liliandaliwa kwa ushirikiano wa makampuni mawili: Lonagro na Seedco, lilifanyika katika mashamba yaliyoko Oljoro. Waandaaji walionesha tekinolojia mpya na mbinu bora za kilimo. Mathalani: Kilimo Hifadhi kwenye zao la mahindi. Miongoni mwa teknolojia kwenye kilimo zilizooneshwa ni; combine harvester, iliyotumika kuonyesha namna ya kuvuna kisasa.

**A C T**

**JARIDA**

**Toleo Maalumu**

# ACT YARATIBU KONGAMANO LA CHAKULA DUNIANI

Tarehe 7 Juni 2021, Baraza la Kilimo Tanzania - (ACT) liliandaa kongamano kuhusu Ubora na Usalama wa Chakula Duniani lililofanyika mjini Morogoro. Kaulimbiu ya kongamano hiyo ilikuwa: ***Ongezeko la Watu, Usalama wa Chakula na Utunzaji wa Mazingira Alisia: Je Wazalishaji Wanasemaje?*** Lililenga kuibua mijadala kuhusu uzalishaji wa chakula kukidhi ongezeko la watu kwa kuzingatia ubora, usalama, viwango vya lishe na utunzaji wa mazingira.

Kongamano hilo, lilijikita kwenye hoja ya Umoja wa Mataifa kuhusu kuongezeka kwa mahitaji ya chakula pamoja na bidhaa nyingine zinazotokana na kilimo. Inakadiriwa kwamba, ifikapo mwaka 2050 idadi ya watu duniani itafikia billioni 9. Je, wakulima wamejiandaa kuweza kukidhi mahitaji ya idadi hiyo? Kongamano hilo lilitoa mapendekezo yatakayowasilishwa katika Mkutano wa Umoja wa Taifa kuhusu Mifumo ya Chakula, utakaohudhuriwa na wakuu wa nchi, mwezi Novemba 2021.



Picha ya wadau walioshiriki kongamano la Chakula Duniani, Morogoro

## WADAU WA ALIZETI WAKUTANA MOROGORO

Tarehe 9 Juni 2021 ACT na taasisi iitwayo Mfuko wa Kuendeleza Soko la Mazao ya Kilimo-AMDT walikutana na wadau wa zao la alizeti mjini Morogoro kujadili kwa kina changamoto katika uzalishaji wa zao hili. Warsha hiyo ilihudhuriwa na wawakilishi kutoka Serikalini, sekta binafsi, makampuni ya mbegu, na wawakilishi wa wakulima. Kaulimbiu ya kikao hicho ilikuwa**: *"Mchango wa zao la alizeti katika kukidhi mahitaji ya mafuta ya kula nchini"*.**

Washiriki wa warsha hiyo walijadili jitihada zinazofanywa na washirika watatu kwa pamoja (yaani Serikali, sekta binafsi, na wabia wa maendeleo) ili kupanua uzalishaji wa zao hili, wakati huohuo, kupunguza changamoto zilizopo. Pia walipendekeza hatua mahususi za kuchukuwa. Kubwa zaidi, waliishauri Serikali idumishe ushuru wa forodha (*import tariff*) kwenye mafuta yanayoagizwa kutoka nje, kwa lengo la kulinda bidhaa hii inayozalishwa nchini mwetu.



**ACT**
**MKUTANO WA WADAU WA ALIZETI,FLOMI HOTEL , MOROGORO 9 JUNI 2021**

## SHEREHE YA MAVUNO YAADHIMISHWA MKOANI RUKWA

Watumishi watatu kutoka Baraza la Kilimo Tanzania: Bi. Jacqueline Edmound, Bi. Edna Theonas, na Bw. Obed Abraham walishiriki kwenye "***Sherehe ya Mavuno"*** iliyofanyika kwa siku mbili, tarehe 13 na 14 Juni 2021, wilayani Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa. Lengo la sherehe hiyo ilikuwa kuelimishwa wadau kuhusu mbinu na maarifa ya uzalishaji wenye tija, pia kuelezea ubora wa mbegu za mahindi DEKALB. Tukio hilo lililopewa jina la ***Kilimo Bora – Maisha Bora,*** lilifadhiliwa na kampuni ya Bayer Crop Science (Tanzania).



# UBALOZI WA NORWAY WATEMBELEA SEKRETARIATI YA ACT

Tarehe 7 June 2021, maafisa kutoka Ubalozi wa Norway, wakiongozwa na Bi. Ingvild Langhus (Mshauri, Mazingira, Mabadiliko ya tabianchi na Maliasili) walitembelea Ofisi za ACT kwa lengo la kufahamiana, pia kujadiliana kuhusu mradi ambao unafadhiliwa na Serikali ya Norway kwa kipindi cha miaka mitatu (2020 - 2023), unaojulikana kwa jina la "***Ubia wa Mradi - Panda Hadhi".***

Mradi huu ni matokeo ya ushirikiano kati ya wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani kutoka Sekta ya Umma, ya Binafsi, na Wabia wa Maendeleo. Mradi huu unatekelezwa katika mikoa 16: Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Morogoro, Dodoma, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga na Simiyu. Mradi huu unaratibiwa na Baraza la Kilimo Tanzania.



**Watumishi wa ACT, wakiwa kwenye picha ya Pamoja na ujumbe kutoka Ubalozi wa Norway nchini**

## JUKWAA LA WACHAMBUZI WA SERA LAKUTANA NA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO

Tarehe 28 Juni 2021, Jukwaa la Watafiti na Wachambuzi wa Sera linalojumuisha ACT, ANSAF, SAGCOT, AMDT, DALBERG, ASPIRES nakadhalika, lilikutana na Kamati ya Bunge ya Kilimo Jijini Dodoma, kujitambulisha kwa Kamati hiyo, pia kuwasilisha changamoto zinazosibu tasnia ya alizeti kwenye mnyororo wa thamani. Kamati ya Bunge iliongozwa na Mwenyekiti wake, Dk. Christine G. Ishengoma (Mb).

Ziara hiyo ilitokana na azimio la Jukwaa lililotolewa kwenye kikao cha tarehe 9 Juni 2021, mjini Morogoro. Wana-jukwaa wakiongozwa na Bw. Timoth Mmbaga, Mkurugenzi Mtendaji, Baraza la Kilimo Tanzania – ACT. Walitaja jitihada zinazochukuliwa kwa pamoja na Serikali, Sekta Binafsi, na Wabia wa Maendeleo kuhakikisha nchi inazalisha mafuta kutosheleza mahitaji yetu, kuuza ziada nje ya nchi. Jukwaa liliwasilisha mapendekezo makuu mawili

- **i.** Kamati isisitize suala la kudumisha Ushuru wa Forodha (*import tariff*), kwenye mafuta ya kula yanayoingizwa kutoka nje ya nchi. Hatua hii italinda wakulima na viwanda vilivyojikita kwenye tasnia ya alizeti.
- ii. Kamati iunge mkono kupitia Bungeni wazo la kuanzisha kilimo cha mkataba (*contract farming*) katika maeneo yanayozalisha alizeti kwa wingi.



**Wanajukwaa wakiwa kwenye picha ya pamoja na Kamati ya Bunge ya Kilimo**

## PICHA YA SIKU



**Mwenyekiti wa ACT (Dr. Jacqueline Mkindi) akijadili jambo na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Majaliwa K. Majaliwa)**




**Mkurugenzi Mtendaji wa ACT akifungua mkutano wa wadau wa alizeti- Morogoro**

JARIDA LA ACT NA. 40|Mei— Agosti 2021

**We Unite. Dialogue. Advocate**

## Dira na Dhamira ya ACT

**Dira**

Kuwa na Sekta ya Kilimo iliyofanikiwa, endelevu na shindani: inayohakikisha usalama wa chakula na lishe unaotokana na msukumo wa kisekta binafsi

**Dhamira**

Kutetea, kuratibu na kuwezesha mazingira rafiki kwa kilimo-biashara.

## Malengo ya ACT

- Kujenga mazingira wezeshi kwa kilimo-biashara
- Kujengea uwezo wanachama wa ACT katika utoaji wa huduma
- Kutuma na kupokea taarifa kutoka wanachama na wadau wengine zinazohusu ustawi wa Sekta ya Kilimo nchini.
- Kuratibu na kuendesha mashirikiano katika ngazi ya taifa na wilaya
- Kuratibu jitihada za Sekta ya Umma na Binafsi katika uendelezaji wa Kilimo-biashara

## *Bodi ya Uhariri*

1. ***Mr. Timoth Mmbaga - Mwenyekiti***
2. ***Mr. Mark Magila- Mjumbe***
3. ***Ms. Laetitia William - Mjumbe***
4. ***Mr. Khalid Ngassa- Mjumbe***
5. ***Mrs. Susan Masagasi- Mjumbe***

## Wasiliana Na.

Mkurugenzi Mtendaji
Agricultural Council of Tanzania
S.L.P 14130,
Dar es
Salaam.

**Simu:** +255 22 2761344,
**Nukushi:** +255 22 2128032
**Barua pepe:** act@actanzania.or.tz
**Tovuti:** www.actanzania.or.tz

# Hii ndo PFS

***Ubia wa Mradi - Panda Hadhi"*** ni matokeo ya ushirikiano kati ya wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani kutoka Sekta ya Umma, ya Binafsi, na Wabia wa Maendeleo. Mradi huu unatekelezwa katika mikoa 16: Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Morogoro, Dodoma, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga na Simiyu. Mradi huu unaratibiwa na Baraza la Kilimo Tanzania.

## Malengo ya Mradi

**Lengo kuu ni;**Kuongeza usalama wa chakula na lishe, na kupunguza umasikini. Umaskini unatarajiwa kupungua kwa 17%, halikadhalika na ukosefu wa lishe kwa watoto kupungua kwa 5%.

## Utaratibu wa Utekelezaji

Mradi utatumia mbinu ya ubia katika utekelezaji wa mradi. Mradi wa PFS, chini ya Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) utaratibu na kuongeza uwezeshaji na utekelezaji ili kuhakikisha ubia unaimarishwa na mafanikio tarajiwa yanafikiwa.

Mradi unatumia ujuzi na maarifa ili kutatua vikwazo muhimu kwenye mnyororo wa thamani. Mradi umeainisha Asasi za Kiraia 35, wabia kutoka setka ya umma na binafsi (ndani na nje ya nchi), wenye uwezo na majukumu mbalimbali watakaoshirikishwa katika kazi ya ubia

## PFS inawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi wa ACT